



MWAKA WA 81
TOLEO NA. 49

8 Desemba, 2000

GAZETI

BEI SH. 200/=

LA

DAR ES SALAAM

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Linatolewa kwa Idhini ya Serikali na
Kuandikishwa Posta kama
Gazeti

YALIYOMO

Taarifa ya Kawaida	Uk
Notice re-Supplement	Na. 843 599
Kupotea kwa Hati ya Kumiliki Ardhi	Na. 844-6 599-600
Muunganisho wa Wadhamini.....	Na. 847-56 600-1

Taarifa ya Kawaida	Uk
Minutes of the Meeting of the Board of	
Directors	Na. 857-8 601-2
Uchunguzi wa Migogoro ya Kikazi	Na. 859-61 602-11
Uthibitisho na Usimamizi wa Mirathi	Na. 862 612
Deed Poll	Na. 863 612

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 843

Notice is hereby given that Regulations and a Notice as set out below, have been issued and are published in Subsidiary Legislation Supplement No. 46 dated 8th December, 2000 to this number of the *Gazette*:-

Regulations under the Tanzania Cotton Lint and Seed Board Act, 1984 (Government Notice No. 471 of 2000).

Notice under the Standards Act, 1975 (Government Notice No. 472 of 2000).

TAARIFA YA KAWAIDA NA 844

KUPOTEA KWA HATI YA KUMILIKI ARDHI

Sheria ya Uandikishaji wa Ardhi

Sura 334

Hati Nambari: 186072/4.

Mmilikaji Aliyeandikishwa: Pure Drinks Limited.
Ardhi: Plot No. 66, Pugu Road, Dar es Salaam.

TAARIFA IMETOLEWA kwamba Hati ya kumiliki Ardhi iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa Hati mpya badala yake iwapo hakuna kipingamizi kwa muda wa miezi miwili tokea tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika *Gazeti* la Serikali.

HATI ya awali ikiionekana lazima irudishwe kwa Msajili wa Hati, Idara ya Hati za Ardhi, S.L.P. 1191, Dar es Salaam.

Dar es Salaam,
19 Oktoba, 2000

T. S. MWAKILEMA,
Msajili wa Hati

Matangazo yahusuyo mali za watu waliofariki, kuvunja mikataba ya ushirikiano na mengineyo, yakiwa ya manufaa kwa umma yawenza kuchapishwa katika *Gazeti*. Yapelekwe kwa Mhariri, Idara Kuu ya Utumishi—Ofisi ya Rais, S.L.P. 2483, Dar es Salaam, Simu za Ofisi 118531/4. Kabla ya Jumamosi ya kila juma.

TAARIFA YA KAWAIDA NA 845

KUPOTEA KWA HATI YA KUMILIKI ARDHI
Sheria ya Uandikishaji wa Ardhi
 Sura 334

Hati Nambari: 186248/100.

Mmilikaji Aliyeandikishwa: Tanzania National Scientific Research Council.

Ardhi: Land Measuring 41,690 Square Feet Block 44 Area 16 Kijitonyama, Dar es Salaam.

Mwombaji: COSTECH.

TAARIFA IMETOLEWA kwamba Hati ya kumiliki Ardhi iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa Hati mpya badala yake iwapo hakuna kipingamizi kwa muda wa miezi miwili tokea tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika *Gazeti la Serikali*.

HATI ya awali ikionekana lazima irudishwe kwa Msajili wa Hati, Idara ya Hati za Ardhi, S.L.P. 1191, Dar es Salaam.

Dar es Salaam,
 19 Oktoba, 2000

T. S. MWAKILEMA,
Msajili wa Hati

TAARIFA YA KAWAIDA NA 846

KUPOTEA KWA HATI YA KUMILIKI ARDHI
Sheria ya Uandikishaji wa Ardhi
 Sura 334

Hati Nambari: 40080.

Mmilikaji Aliyeandikishwa: Restansgar Mlale.

Ardhi: Kiwanja Na. 404 Kitalu 'E' Tegeta, Jijini Dar es Salaam.

TAARIFA IMETOLEWA kwamba Hati ya kumiliki Ardhi iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa Hati mpya badala yake iwapo hakuna kipingamizi kwa muda wa miezi miwili tokea tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika *Gazeti la Serikali*.

HATI ya awali ikionekana lazima irudishwe kwa Msajili wa Hati, Idara ya Hati za Ardhi, S.L.P. 1191, Dar es Salaam.

Dar es Salaam,
 6 Juni, 2000.

T. S. MWAKILEMA,
Msajili wa Hati

TAARIFA YA KAWAIDA NA 847

MUUNGANISHO WA WADHAMINI
Sheria ya Muunganisho wa Wadhamini
 (Sura ya 375)

Taarifa inatolewa ya kuwa kufuatana na kifungu cha 3(1) cha Sheria ya Muunganisho wa Wadhamini inatolewa Shahada ya Muunganisho wa Wadhamini kwa jina lifuatalo:

THE REGISTERED TRUSTEES OF CONGREGATION OF THE CAPUCHIN TERTIARY SISTERS OF THE HOLY FAMILY

Dar es Salaam,
 13 Julai, 2000

C. O. KAISI,
Msimamizi Mkuu wa Wadhamini

TAARIFA YA KAWAIDA NA 848

MUUNGANISHO WA WADHAMINI
Sheria ya Muunganisho wa Wadhamini
 (Sura ya 375)

Taarifa inatolewa ya kuwa kufuatana na kifungu cha 3(1) cha Sheria ya Muunganisho wa Wadhamini inatolewa Shahada ya Muunganisho wa Wadhamini kwa jina lifuatalo:

THE REGISTERED TRUSTEES OF TRAINING AND CONSULTANCY CENTRE "TRACE"

Dar es Salaam,
 13 Aprili, 2000

C. O. KAISI,
Msimamizi Mkuu wa Wadhamini

TAARIFA YA KAWAIDA NA 849

MUUNGANISHO WA WADHAMINI
Sheria ya Muunganisho wa Wadhamini
 (Sura ya 375)

Taarifa inatolewa ya kuwa kufuatana na kifungu cha 3(1) cha Sheria ya Muunganisho wa Wadhamini inatolewa Shahada ya Muunganisho wa Wadhamini kwa jina lifuatalo:

THE REGISTERED TRUSTEES OF THE ABANTU VISIONS TRUST

Dar es Salaam,
 14 Septemba, 1999

C. O. KAISI,
Msimamizi Mkuu wa Wadhamini

TAARIFA YA KAWAIDA NA 850

MUUNGANISHO WA WADHAMINI
Sheria ya Muunganisho wa Wadhamini
 (Sura ya 375)

Taarifa inatolewa ya kuwa kufuatana na kifungu cha 3(1) cha Sheria ya Muunganisho wa Wadhamini inatolewa

Shahada ya Muunganisho wa Wadhamini kwa jina lifuatalo:

THE REGISTERED TRUSTEES OF ASILIA TRUST FUND

Dar es Salaam,
4 Februari, 2000

C. O. KAISI,
*Msimamizi Mkuu wa
Wadhamini*

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 851

MUUNGANISHO WA WADHAMINI
Sheria ya Muunganisho wa Wadhamini

(Sura ya 375)

Taarifa inatolewa ya kuwa kufuatana na kifungu cha 3(1) cha Sheria ya Muunganisho wa Wadhamini inatolewa Shahada ya Muunganisho wa Wadhamini kwa jina lifuatalo:

REGISTERED TRUSTEES OF WOMEN INITIATIVE FOR THE STREET AND WORKING CHILDREN WELFARE (WIWOCHI)

Dar es Salaam,
12 Aprili, 2000

C. O. KAISI,
*Msimamizi Mkuu wa
Wadhamini*

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 852

MUUNGANISHO WA WADHAMINI
Sheria ya Muunganisho wa Wadhamini

(Sura ya 375)

Taarifa inatolewa ya kuwa kufuatana na kifungu cha 3(1) cha Sheria ya Muunganisho wa Wadhamini inatolewa Shahada ya Muunganisho wa Wadhamini kwa jina lifuatalo:

THE REGISTERED TRUSTEES OF KIMBAU DEVELOPMENT FUND

Dar es Salaam,
22 Machi, 2000

C. O. KAISI,
*Msimamizi Mkuu wa
Wadhamini*

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 853

MUUNGANISHO WA WADHAMINI
Sheria ya Muunganisho wa Wadhamini

(Sura ya 375)

Taarifa inatolewa ya kuwa kufuatana na kifungu cha 3(1) cha Sheria ya Muunganisho wa Wadhamini inatolewa Shahada ya Muunganisho wa Wadhamini kwa jina lifuatalo:



KANISA LA PENTEKOSTE OLDEAN MBULU

Dar es Salaam,
28 Aprili, 2000

C. O. KAISI,
*Msimamizi Mkuu wa
Wadhamini*

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 854

MUUNGANISHO WA WADHAMINI
Sheria ya Muunganisho wa Wadhamini

(Sura ya 375)

Taarifa inatolewa ya kuwa kufuatana na kifungu cha 3(1) cha Sheria ya Muunganisho wa Wadhamini inatolewa Shahada ya Muunganisho wa Wadhamini kwa jina lifuatalo:

THE REGISTERED TRUSTEES OF MASJIDUL ISTIQAMAH-MZAMBARAUNI

Dar es Salaam,
3 Mei, 2000

C. O. KAISI,
*Msimamizi Mkuu wa
Wadhamini*

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 855

MUUNGANISHO WA WADHAMINI
Sheria ya Muunganisho wa Wadhamini

(Sura ya 375)

Taarifa inatolewa ya kuwa kufuatana na kifungu cha 3(1) cha Sheria ya Muunganisho wa Wadhamini inatolewa Shahada ya Muunganisho wa Wadhamini kwa jina lifuatalo:

THE REGISTERED TRUSTEES OF TANZANIA ADVENT YOUTH AGENCY (TAAYO)

Dar es Salaam,
7 Aprili, 2000

C. O. KAISI,
*Msimamizi Mkuu wa
Wadhamini*

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 856

MUUNGANISHO WA WADHAMINI
Sheria ya Muunganisho wa Wadhamini

(Sura ya 375)

Taarifa inatolewa ya kuwa kufuatana na kifungu cha 3(1) cha Sheria ya Muunganisho wa Wadhamini inatolewa Shahada ya Muunganisho wa Wadhamini kwa jina lifuatalo:

REGISTERED TRUSTEES OF USAMBARA LISHE TRUST (U.L.T)

Dar es Salaam,
30 Machi, 2000

C. O. KAISI,
*Msimamizi Mkuu wa
Wadhamini*

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 857

MINUTES OF THE MEETING OF THE BOARD OF DIRECTORS HELD ON 15TH MAY, 2000 AT THE REGISTERED OFFICE OF THE COMPANY AT 11.00 A.M

Present: Mr. Shakir Mohamedraza Sherally - Director in chair
Mr. Yusuf Gulamali Mohamed Kermali - Director

Mr. Mohamed Gulamhussein Lalji - Secretary

Min. No. 1:

Winding up of the Company

It was resolved that the Company be wound up immediately as it was not operational.

CONFIRMED

Chairman

Secretary

15th May, 2000

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 858

MINUTES OF THE MEETING OF THE BOARD OF DIRECTORS HELD ON 27TH MAY 2000 AT THE REGISTERED OFFICE OF THE COMPANY AT 10.00 A.M.

Present: Mr. Hasnain Punja - Chairman
Mrs. Umulbanin Punja - Director
Miss. Faiza Punja - Director

Min. No. 1:

Winding up of the company

It was resolved that the Company be wound up immediately.

CONFIRMED

HASNAIN PUNJA
Chairman

FAIZA PUNJA
Director

27th May 2000

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 859

MGOGORO WA UCHUNGUZI NA. 32 YA 1996
baina ya
S. B. KADEGE - DAR ES SALAAM
na
TANZANIA BREWERIES LTD. - DAR ES SALAAM
UAMUZI

Mgogoro huu wa Uchunguzi baina ya Bwana Sylvester Bernard Kadege dhidi ya Tanzania Breweries Ltd. ulianza kusikilizwa katika Mahakama hii mnamo tarehe 3 Novemba, 1997.

Kamishna wa Kazi alipoleta Mgogoro huu wa Uchunguzi ameomba Mahakama kufanya uchunguzi mambo yafuatayo:-

(a) Uhalali wa sababu zilizofanya Bwana Sylvester B. Kadege aachishwe kazi,

- (b) Kama taratibu za kisheria zilifuatwa wakati v kumuachisha kazi,
- (c) Masuala mengine yoyote yaliyojitekeza katil Mgogoro huu.

Katika uchunguzi huu Bwana Sylvester Kadege aliongozwa na Wakili Rutabingwa wakati akitoa ushahidi wake. Bwana Kadege alieleza Mahakama kama ifuatavy

Aliajiriwa na Tanzania Breweries Ltd. mnamo tarehe 1/9/83 kama Afisa Usalama daraja la kwanz Alithibitishwa Kazini mnamo tarehe 29/2/84. Mnamo tarehe 10/9/94 alipandishwa Cheo kuwa Meneja Usalama katika Kampuni. Kazi yake kama Meneja Usalama v Kampuni ni kuendesha shughuli za Ulinzi kuhakikis usalama wa mali. Bwana Kadege ameeliaza kuwa alikuwa anawajibika kwa Meneja wa Kiwanda cha Dar es Salaam Mnamo tarehe 22/12/95 kulitokea wizi wa carton Bia makopo aina ya Castle. Tarehe 27/12/95 aliandikiwa barajieze jinsi wizi huo uliyotokea na namna ya kuwamikakati ya kuzuia wizi wa namna hiyo. Alijibu na kui mapendekezo yake mnamo tarehe 2/1/96. Mnamo Februari 1996, Meneja wake alimuandikia tathmini ya Utendaji K: wake (performance appraisal). Katika tathmini hiyo Meneja wake alionyesha kwamba kulikuwa na wizi mwirikiwandani na alipendekeza Bwana Kadege aondole katika wadhifa wake kama Meneja Usalama. Kwa kipir hicho hapakuwa na wizi wowote uliyotokea. Tathmini Meneja wake ilikuwa ya kuanzia 1 Julai, 1995 hadi tarehe 31 Desemba, 1995. Bwana Kadege alisema hakukubaliana tathmini hiyo na aliandika kutokubaliana na hi tathmini kwenye Tathmini yenye. Bwana Kadege alisema kuwa alilalamika kwa "Executive Director Technical" ambaye anahusika na kuzalishaji. "Executive Director Technical" alikubali kuwaita yeeye na Meneja Kiwanda (Plant Manager) ili ijulikane ni vipi Menamefikia Tahtmini hiyo. "Executive Director" alikuwa Mkuu wao wa Idara. Iliundwa Tume ya kuchunguza h Tathmini ya Meneja. Tume hiyo ilikuwa ya "Executive Director Technical" na "Human Resources Director". Mnamo tarehe 18/3/96 Bwana Kadege aliiwa kwenye Turia alihojiwa. Baada ya kuhojiwa tume ilikubaliana mapendekezo ya Meneja wa Kiwanda. Bwana Kadege alijulishwa kwa maandishi kwa barua ya tarehe 21/3/96. Baada ya kujulishwa kwa maandishi kuhusu matokeo uchunguzi wa Tume, alihamishiwa katika Garage akateremshwa cheo na kuwa "Security Officer External". Bwana Kadege ameeliaza kuwa aliathirika kwa uamuzi h kwani mshahara wake ulipunguzwa. Kabla ya tukio h alikuwa anapata mshahara wa Tshs. 210,000/= alipoondolewa wadhifa wa Umeneja Usalama akawa anapata mshahara Tshs. 155,000/=. Hata hivyo mnamo tarehe 7/96 Mnejimenti iliandika barua ya kufuta Uamuzi wake kumpunguza cheo (Demotion). Pamoja na barua hiyo Bwana Kadege ameeliaza zaidi kwamba aliendelea kuwa "Security Officer External" lakini mshahara pia haukubadilika ha alipolalamika. Mnamo tarehe 1/4/96 aliandikiwa bar kuwa kwa nini asiachishwe kazi kwa kutofanya kinaavyopashwa. Katika barua hii Tuhuma ilikuwa ni ile

mwanzo. Barua hii iliandikwa na Mkurugenzi wa umishi ambaye alikuwepo kwenye Tume ya Uchunguzi. wana Kadege alijibu barua hiyo mnamo tarehe 3/4/96 ikiwa tkiambatanisho kuonyesha matukio ya 1994 ukilinganisha 1995, ambayo kulikuwa na upungufu. Baada ya kupeleka alezo yake, mnamo tarehe 4/4/96 alipewa barua ya usimamishwa kazi mnamo tarehe 9/4/96 aliandikiwa barua kumtaka ahudhurie Kikao cha "Executive Board" kwa tarehe 11/4/96. Alihojiwa na "Executive Board" na mnamo tarehe 12/4/96 aliandikiwa barua ya kumuachisha kazi. atika kutoa ushahidi wake Bwana Kadege alitoa vielelezo Tanzania P.1 hadi P. 15 ambazo ni nyaraka mbalimbali kama ivyokuwa akitaja tarehe zake na kinachofuata. Bwana adege alisitisiza kuwa Wajumbe amba walikuwa kwenye jme walishiriki kumhoji. Katibu wa Kikao hicho alikuwa Mkurugenzi wa Utumishi ambaye alikuwa Mjumbe wa ume. Bwana Kadege amedai zaidi kuwa baada ya kumaliza ahojiano aliruhusiwa kuondoka lakini Wajumbe wa Tume iwaacha ndani. Baada ya kuachishwa kazi alikwenda ilalamika OTTU Tawi na ndipo taratibu za Mgogoro huu lianza hadi kufika hapa Mahakama. Kwa kumalizia shahidi wake Bwana Kadege aliiambia Mahakama hii wamba utaratibu wa Ulinzi ulikuwa chini yake na vile vile ilikuwa na "Supervisors" pia kulikuwepo na Kampuni ya linzi ya nje iliyokodishwa kulinda Mameneja huko ajumbani. Bwana Kadege ameiomba Mahakama ipokee alezo yake na itengue Uamuzi wa Mwajiri wa kumuchisha azi. Ameomba arudishwe kazini na alipwe haki -azostahili ambazo Mahakama hii itaona zinafaa.

Upande wa utetezi/mlalamikiwa ultakiwa kuleta ushahidi ujibu hoja ya malalamiko ya Mlalamikaji, na ulileta shahidi imoja ambaye ni Bwana Robert Charles Mwaimu (DW 1) wana Mwaimu akiongozwa na Wakili wa Utetezi Bwana Thibert Tenga alieleza Mahakama hii kwamba; yeye nafanya kazi katika Kampuni ya Bia Tanzania (TBL) kama Corporate Industrial Relations Manager". Kabla ya hapo ilikuwa "Executive Director Human Resources". Alikuwa

Director wa Human Resources" kuanzia tarehe 1/1/94. namfahamu Bwana Kadege ambaye ni Mlalamikaji kwamba iwhi kuwa "Security Manager" wa Kampuni ya Bia. liachishwa kazi mwaka 1996. Sababu za kuachishwa kazi i kutohakana na "performance appraisal" aliyofanyiwa na Mkuu wake wa Kazi. Kielelezo P.6 alichotoa Mlalamikaji utumika kuangalia tathmini ya utendaji kazi wa mfanyakazi. ielezo hicho P.6 kilihusu Tathmini ya kuanzia Julai, 1995 adi Desemba, 1995. Baada ya "appraisal" hiyo kufanyika wana Kadege hakukubaliana nayo. Bwana Kadege alipeleka mlalamiko yake ngazi ya juu. Kwa kuwa Mkuu wake na eye mwenyewe wote ni Mameneja, aliteuliwa Mkurugenzi -a Uhndisi - "Executive Director Technical", Bwana Paul Scott Crossely kushughukia suala la Bwana Kadege na Mkuu wake Meneja Kiwanda. Bwana Mwaimu alieleza kuwa Bwana Kadege na Meneja wake waliitwa kwenye Tume ya Uchunguzi ambapo yeye Bw. Mwaimu alikuwa anaandika Miniti kama Katibu. Kwa maoni ya Meneja wake ni kwamba Bwana Kadege hakuwa na uwezo wa kufanya kazi kama lityotegemewa. Katika kikao hicho cha Uchunguzi hatimaye Bwana Kadege alitaarifiwa kuwa Tathmini ya Utendaji Kazi

wake aliyofanyiwa na Kiongozi wake ilikuwa sahihi. Bwana Kadege vile vile alitwa kujieleza katika Kikao cha nidhamu na ajira ambayo ni "Executive Board". Katika Kikao hicho mambo yaliyozungumziwa ni kuona ni nani kati ya Kadege na Meneja wake alikuwa shahidi katika Tathmini ya Utendaji kazi wa Bwana Kadege. Bwana Kadege alifanyiwa Tathmini ikiwa ni utaratibu wa Kampuni ambayo hufanywa kwa mwaka. Viongozi wote hufanyiwa "Assesment" na Wakuu wao. Matokeo ya Tume ya Uchunguzi ilikuwa kwamba Tathmini ya Meneja Mitambo ilikuwa sahihi. Katika uchunguzi wa Tume Bwana Kadege alikiri kwamba wafanyakazi waliokuwa chini yake hawakufuata taratibu za kudhibiti matukio ya jinai. Kulikuwa na mtazamo kwamba Idara ya Usalama (security) badala ya dhibiti uhalifu ilikuwa inaarifiwa matukio ya uhalifu. Kulikuwa hakuna udhibiti wa Walinzi waliokuwa katika Idara yake. Taarifa ya Kikao cha Tume ya Uchunguzi ilipelekwa kwenye "Executive Board" ikipendekeza Bwana Kadege afukuzwe Kazi. Bwana Kadege aliarifiwa kuwa anawenza kwenda kwenye "Executive Board" akiwa na mtu mwingine ili ajitetee, kwa utendaji dhaifu kutohakana na Tathmini iliyofanyiwa na Meneja Mitambo (Plant Manager). Bwana Mwaimu alitoa Miniti za Kikao cha "Executive Board" kama kielelezo D. 2 cha tarehe 11/4/96. Katika kikao hicho Bwana Mwaimu alihudhuria kama Mjumbe na Mwandishi wa Miniti. Baada ya Bwana Kadege kuhojiwa, alisema yeye Bwana Mwaimu, "Plant Manager" na "Executive" na kutoa Uamuzi. Uamuzi wa "Board" ilikuwa kwamba Bwana Kadege aachishwe Kazi. Bwana Mwaimu alimaliza ushahidi wake kwa kusema kwamba kwa maoni yake taratibu zote zilitumika ipasavyo na kwamba ilikuwa haki na halali kumuachisha Kazi Bwana Kadege. Ameona "Chart" ya Bwana Kadege kuhusu kushuka kwa matukio ya jinai, lakini hakubaliani nayo kwa sababu "Chart" hiyo haikusaidia kujibu hoja ya utendaji wake wa kazi. Bodi iliama Bwana Kadege aachishwe kazi kuitia kielelezo P.15 kuanzia tarehe 12/4/96. Huu ukawa ndiyo mwisho wa ushahidi kwa upande wa Utetezi.

Ingawa nilianza kusikiliza Mgogoro huu wa Uchunguzi nikiwa na Washauri wa Mahakama, lakini sikubahatika kupata maoni yao kwani hawakuweza kuhudhuria Mahakama wakati Shauri hili linafikia ukingoni. Hata hivyo fungu la 19(3) la Sheria Na. 3 ya 1990 ya Mahakama ya Kazi linaniruhusu kutoa Uamuzi bila kupata maoni ya Washauri kwa kutohudhuria kwao Mahakama. Ni wajibu wangu kulitolea Uamuzi shauri hili.

Ushahidi uliotolewa na upande wa Mlalamikaji Bwana Kadege na ule wa Utetezi uliotolewa na Shahidi Bwana Mwaimu, kimsingi hautofautiani. Mlalamikaji alifanyiwa Tathmini ya Utendaji Kazi wake na Mkuu wake, Meneja Mtambo wa Dar es Salaam. Utaratibu huu hutumika katika Kampuni ya Bia kupima uwezo wa mfanyakazi kutimiza majukumu yake ya kazi hasa akiwa kiongozi wa Idara. Utaratibu huu haukupingwa na Mlalamikaji kwamba haupo. Ushahidi wa Mlalamikaji unaonyesha kuwa kwa wakati huo katika kipindi cha mwaka 1994/95 kumekuwa na matukio ya wizi na tukio kubwa lilikuwa la wizi wa Carton za bia aina ya Castle. Mlalamikaji ameleeza Mahakama kwamba aliandikiwa barua na Meneja Mtambo ambaye ni Mkuu

wake mnamo tarehe 27/12/95 ajieleze jinsi wizi huo uliyotokea na aweke mikakati ya jinsi ya kuzuia wizi huo usitokee hapo baadaye. Barua hiyo ni kielelezo P. 4. Hata hivyo Mkuu wake wa Kazi alimfanyia Tathmini ya Utendaji wake wa Kazi na akaonekana kuwa Utendaji wake wa Kazi upo chini ya matarajio ya Kiwanda/Kampuni na kwa hali hiyo Meneja wake alipendekeza Mlalamikaji aondolewe katika wadhifa wake. Tathmini ilifanywa kwa kipindi cha kuanzia tarehe 1 Julai, 1995 hadi tarehe 31 Desemba, 1995. Huu ni utaratibu wa Kampuni kuhusu kuleta ufanisi wa utendaji kazi, uwajibikaji na kulinda mali ya Kampuni kwa upande wa Mlalamikaji kama Meneja Usalama (Security Manager). Ushahidi huu kama nilivyo uelezza uliungwa mkono na Shahidi wa Utetezi Bw. Mwaimu kwamba matukio ya wizi yalikuwepo na kwamba utaratibu wa viongozi wa Idara kufanyiwa Tathmini na viongozi wao wa Kazi ndiyo unaotumika katika Kampuni ya Bia. Mlalamikaji kwa kuwasilisha Mgogoro huu katika Mahakama hii kupitia kwa Kamishna wa Kazi ameona kwamba ameoneawa kwa kitendo cha mwajiri wake kumuachisha kazi.

Kamishna wa Kazi alipoleta Mgogoro huu wa Uchunguzi katika Mahakama hii ameomba Mahakama kufanyia Uchunguzi mambo mawili muhimu:-

- (1) Uhalali wa sababu zilizofanya Bwana Sylvester B. Kadege aachishwe kazi;
- (2) Kama taratibu za kisheria zilitumika wakati wa kumuachisha kazi.

Ili kuweza kujibu hoja hizo za Kamishna wa Kazi ambazo zinapashwa kutolewa Uamu, ni vizuri kuangalia nini kilifuata baada ya Tathmini iliyofanywa na Kiongozi wa Bwana Kadege na mapendekezo ya kumvua wadhifa wake.

Upo ushahidi wa Mlalamikaji pamoja na Shahidi wa Utetezi kwamba kwa kutokuridhika na Tathmini ya Mkuu wa Kazi wa Mlalamikaji, iliundwa Tume ya Uchunguzi (Inquiry team) kuona kama Tathmini ya "Plant Manager" ilikuwa sahihi au ilimkandamiza Mlalakaji. Tume ya Uchunguzi ilikuwa chini ya "Executive Director Technical" na Mjumbe mmoja ambaye pia aliandika Miniti Bwana, Mwaimu, shahidi wa Utetezi, wakati huo akiwa "Executive Director Human Resources". Mlalamikaji aliiwtwa pamoja na Mkuu wake - "Plant Manager" na wakahojiwa kuhusu Tathmini iliyofanyika ili kujua ni nani kati yao yuko sahihi. Kielelezo D 1 Miniti za Kikao cha Tume chahusika. Baada ya kuhojiwa wahusika hao wawili, Tume ya Uchunguzi ilikuwa na mtazamo kama ifuatavyo na ninanukuu:-

"2(i) Reading from the graph only one case has been reported between July - December, 1995. There seems to be a confusion of mixing up Criminal with ordinary disciplinary issues. The graph does not prove that Crime rates fell between July - December, 1995.

3.2 By Security Manager's own admission the department's employees do not adhere to laid down rules. This signifies management's fault. A good example is lack of control of the security vehicle.

3. There is a clear indication that the security department only reacts after an event has taken place and reports on thefts etc. are done by people outside the security unit. This signifies inefficiency.

4. A clear example of lack of Management control is where the security guard was caught filling up overtime claims for others.

Huo ndiyo mtazamo (observations) wa Tume, kwamba inaunga mkono Tathmini ya "Plant Manager" kutokana na yote yaliyonukuliwa hapo juu 3(1) - 2.hadi 6. Upo vile vile ushahidi wa pande zote mbili kwamba licha ya mtazamo wa Tume, suala hili lilipelekwa kwenye "Executive Board" kwa kuwa kulikuwa na mapendekezo ya kusitisha ajira ya Bwana Kadege, kutokana na Tathmini iliyofanywa na "Plant Manager" na kuungwa mkono na Tume ya Uchunguzi. Bwana Kadege aliiwtwa kwenye Kikao cha "Executive Board" kilichofanyika tarehe 11/4/96. Katika kikao hicho Bwana Kadege alifahamishwa yafuatayo na ninanukuu:

"3.Q.

Mr. Kadege, you are aware of the purpose of this meeting. We are here to deliberate on whether to agree with the Management intention to terminate your service from the Company or otherwise. You know the history of the case, how it began by your disagreeing with the awarded ratings given by your supervisor, the Plant Manager (DSM) and the Inquiry that followed plus the latter opinion that the Plant Managers assessments as appraisal form is fair. Are you aware of this?

A: Yes I am aware.

Q: You are also aware that the Management had written to you asking you to be accompanied with a TBL employee of your choice to act as your witness during the hearing of your defence. Is that so?

A: Yes it is so but I did not bring any because I trust that the Board will be fair.

Q: Before you are Mr. P. Scott - Crossley, B. Harries, R. Rweyemamu, C.R.S. Mwaimu, Mrs. R. Adam, B. Semfukwe and myself Mr. Kilewo. Is there any body in this room you feel should not participate in the hearing of your Case?

A: No"

Iliyonukuliwa hapo juu ni sehemu ya Miniti za Kikao hicho cha "Executive Board" ambapo Bwana Kadege alifahamishwa nini madhumuni ya Kikao hicho kama alikuwa ana taarifa, na haki zake za kimsingi.

Baada ya uchambuzi nilioufanya hapo juu sasa ni wakati muafaka wa kujibu hoja za Kamishna wa Kazi. Hoja ya kwanza inahusu "Uhalali wa sababu zilizofanya Bwana Sylvester B. Kadege aachishwe kazi". Ushahidi unaonyesha kuwa Bwana Kadege alipewa dhamana katika Ajira yake kuwa Meneja Usalama. Ushahidi unaonyesha kulikuwa na matukio mengi ya wizi ambayo ingekuwa sahihi zaidi kama yangegunduliwa na kutolewa taarifa na Kitengo chake lakini matukio hayo yalikuwa yakigundulika na kutolewa taarifa na watu wa vitengo vingine ambaa siyo kitengo cha

Usalama. Imedhihirika kwamba ni utaratibu kwa wakuu wa Idara kufanyiwa Tathmini ya Utendaji kazi katika Kampuni ya Bia. Inapodhihirika kwamba aliyefanyiwa Tathmini ameonekana utendaji kazi wake upo chini ya matarajio na malengo ya Kampuni ni hatua gani zinapashwa kuchukuliwa dhidi yake? Je abakizwe kwenye ajira ambayo ye ye mtathminjiwa hakidhi haja ya matakwa ya Kampuni? Jibu ni hapana. Bwana Kadege alielezwa kuhusu Tathmini iliyofanywa dhidi yake na alipewa nafasi ya kuomba rufaa ambapo Tume ya Uchunguzi iliundwa na ambayo mtazamo wake nilikwisha ueleza hapo awali. Bwana Kadege alioneckana kwamba haimudu kazi ambayo aliajiriwa katika wadhifa wa Meneja Usalama wa Kampuni. Sababu ya kumuachisha kazi Bwana Kadege ni kutokuimudu kazi ambayo ameajiriwa na Kampuni. Ni dhahiri kabisa kwamba mtu yeyote ambaye haimudu kazi yake hana sababu ya kuendelea na Ajira. Ni uamuzi wangu kwamba kutokuimudu kazi uliyoajiriwa kufanya ni sababu halali ya kukufanya uachishwe kazi. Shauri la Bwana Kadege ni tofauti kabisa na mashauri mengine ambayo yanahusu utovu wa nidhamu katika ajira au tuhuma zeny mwelekeo wa kijinai. Shauri hili linahusu utendaji kazi chini ya kiwango kinachokubalika katika Ajira ya Kampuni. (If the standard of performance is not met what next?). Kama kiwango cha utendaji kazi alijoajiriwa mtu kufanya hakikufikiwa nini kifuate? Kwa hali hiyo hoja ya kwanza ya Kamishna wa Kazi imejibiwa.

Hoja ya pili ya Kamishna wa Kazi ni "Kama taratibu za Kisheria zilitumika wakati wa kumuachisha kazi".

Upo ushahidi kwamba Bwana Kadege baada ya Tathmini kufanyika alioneckana kuwa yuko chini ya kiwango kilichotarajiwa na Kiwanda/Kampuni. Bwana Kadege alipewa nafasi, kwanza ya rufaa kipinga Tathmini na Tume ikaundwa na akasikilizwa na mtazamo wa Tume ya uchunguzi na mapendekezo kufanywa na kupelekwa kwenye "Executive Board". Mapendekezo ya Tume yalikuwa ni kwamba, Bwana Kadege afukuzwe kazi. Napenda kunukuu pendekezo la Tume kama liliyopelekwa kwenye "Executive Board".

"2.1.4 The Panel recommended the adoption of alternative 2.1.3 (iii) above because it suits the contractual obligations of the employee where he may not only be terminated by summarily dismissed if his work performance falls below expected standards."

Bwana Kadege alipata nafasi ya pili kwa kuitwa kwenye "Board" ajitetee kwa nini ajira yake isisitishwe katika Kikao cha "Executive Board" cha tarehe 11/4/98. Napenda ninukuu tena sehemu ya ufahamisho alipewa siku alipohudhuria kikao hicho.

Q: Mr. Kadege, you are aware of the purpose of this meeting. We are here to deliberate on whether to agree with the management intention to terminate your services from the Company or otherwise. You know the history of the case, how it began by your disagreeing with the awarded ratings given by your Supervisor,

the Plant Manager (DSM) and the Inquiry that followed plus the latter opinion that the Plant Managers assessment as recorded in the performance appraisal form is fair. Are you aware of this?

A: Yes I am aware"

Bwana Kadege alipewa nafasi ya kujitetea kwenye "Executive Board" ambayo ni mamlaka yake ya Ajira. Na baada ya kuhojiwa na kujitetea kwenye "Board", upo ushahidi kwamba, ye ye mwenyewe na wale wajumbe wa Tume ya Uchunguzi walitolewa nje. Ni vema ninukuu sehemu ya yaliyomo katika Miniti za "Board" kuhusu Wajumbe wa Tume kutolewa nje:-

"Now before we decide on the subject I suggest that the Executive Director (T) and Executive Director (HR) leave the room because the two officers had participated in the initial Inquiry (Exit M/S crossly and Mwaimu at 5.03 pm.)

Baada ya hapo ndipo "Board" ikatafakari na hatimayé kutoa Uamuzi. Kimsingi ni kwamba taratibu za kisheria kuhusu misingi ya haki ya asili ya Bwana Kadege ilifuatwa. (The principals of natural justice were adhere to). Bwana Kadege alipewa nafasi ya kujitetea kwenye Board, na wale waliomtuhumu kwa utendaji kazi wake ulio chini ya matakwa ya Kampuni hawakuwepo wala kushiriki katika maamuzi ya Board ya kumuachisha kazi. Kwa hali hiyo hoja ya pili ya Kamishna wa Kazi imejibiwa.

Kutokana na uchambuzi wa ushahidi na vielelezo nilivyo nukuu kama nilivyoonyesha hapo juu ni uamuzi wangu kuwa malalamiko yaliyopo mbele ya Mahakama hii katika Mgogoro huu wa Uchunguzi hayana misingi na ninayatupilia mbali. Mlalamikaji aliachishwa kazi kwa misingi ya haki na halali na utaratibu uliotumika kumuachisha kazi ulifuata matakwa ya Sheria. Haingeweze kana katika mfumo mpya wa uchumi wa biashara ya ushindani kuvumilia uzembe na kutowajibika mahali pa kazi na kusababisha hasara kwa Kampuni yoyote ile iliyopo katika Ushindani wa Kibashara.

Uamuzi huu umetolewa leo tarehe 15 Juni, 1998, na unakuwa TUZO ya Mahakama. Uamuzi huu umetiwa sahihi na mimi Leo tarehe 15 Julai, 1998 na unakuwa na nguvu ya kisheria.

s.g.d.

J. B. TENDWA
Naibu Mwenyeekiti

Certified true copy of the original.

B. E. NYAMUBI,
Registrar

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 860

**MGOGORO WA KIKAZI NA. 41 WA 1997
baina ya**

V. B. CHIBWANA
na.
CHUO CHA ARDHI

UAMUZI

J. B. Tendwa, DC

Uamuzi huu unatokana na Mgogoro wa Uchunguzi ambao umewasilishwa na Kamishna wa Kazi kwa barua yenye Kumbukumbu KZ/U.10/MG/757/9 ya tarehe 27 Juni 1997, akiiomba Mahakama chini ya fungu^la 8(a) la Sheria ya Mahakama ya Kazi Na. 2 ya mwaka 1993, kufanya uchunguzi mambo yafuatayo:

- (a) Kama uongozi wa Chuo cha Ardhi ulifuata Sheria ya kumuachisha kazi Bw. V. Chibwana.
- (b) Kama hatua za kumwachisha kazi Bw. V. Chibwana zilikuwa za haki kwa mujibu wa Sheria za utovu wa nidhamu.
- (c) Kama kitendo 'Management' cha kubadilisha Mkataba wa Ajira ulikuwa ni halali kwa mujibu wa Sheria za Kazi.
- (d) Kama Sheria nyingine zinazoambatana na Mhusiano kazini zilifuatwa.

Shauri lilianza kusikilizwa na Mh. Mlelwa (Naibu Mwenyekiti mwenzangu) hadi kufikia utetezi ambapo shahidi wa kwanza na wa pili walitoa ushahidi wao na ndipo mnamo tarehe 1/10/98, Bw. Ngulla Mwakilishi wa Mlalamikaji, alipomfahamisha Mh. Mlelwa kama ifuatavyo:

"Ngulla: Naona kuwa Naibu Mwenyekiti una upendeleo (you are biased). Naomba shauri hili lisikilizwe na Mwenyekiti au Naibu Mwenyekiti mwingine"

Mh. Mlelwa baada ya kufahamishwa hivyo na kuombwa asiendelee kusikiliza shauri hili, na yeze alitoa Amri kama ifuatavyo:

"Amri: Kutokana na maoni ya Bw. Ngulla Mwakilishi wa Mlalamikaji yakuwa naonyesha upendeleo katika shauri hili hivyo basi najiondoa ili shauri hili lianze upya au liendelee kusikilizwa na Naibu Mwenyekiti mwingine".

Jalada husika lilipelekwa kwa Mh. Jaji Mwaikasu ambaye alikuwa Mwenyekiti wa Mahakama hii kwa ajili ya kupangiwa Naibu Mwenyekiti ambaye ataendelee kusikiliza shauri hili. Mh. Jaji Mwaikasu, mnamo tarehe 2/10/98, baada ya kupata jalada hilo na yeze alitoa Amri kama ifuatavyo:

"Amri: Kutokana na kujitoe kwa Mh. Mlelwa, DC, kusikiliza uchunguzi huu wa mgogoro wa kikazi, kufuatia madai ya Mwakilishi wa Mlalamikaji kuwa umeonyesha upendeleo katika kuendesha uchunguzi huu, amri inatolewa kwamba kesi hii ya uchunguzi, inahamishiwa kwa Mh. Tendwa, Naibu Mwenyekiti mara moja".

Baada ya hapo shauri liliendelea kutajwa na hatimaye kupangiwa kusikilizwa mnamo tarehe 19/7/99. Kabla ya kuahirishwa shauri hili na hatimaye kuhamishiwa kwangu, Bw. Ngulla alikuwa akimhoji shahidi wa pili ambaye ni Bw. H. S. Matutu. Kwa tarehe hiyo 19/7/99, Bw. Ngulla aliifahamisha Mahakama kuwa amemaliza kumhoji shahidi huyo wa pili wa utetezi na alikubali kuwa shauri liendelee na shahidi watatu wa upande wa utetezi aitwe.

Baada ya kuelezea jinsi shauri lilivyoendelea hadi hapo tarehe 19/7/99, ni vizuri sasa nikauanisha ushahidi wote kadiri uliviyotolewa Mahakamani kwa pande zote mbili yaani upande wa mlalamikaji ambao ulikuwa na shahidi, mmoja tu na upande wa utetezi ambao ulileta mashahidi watatu.

Katikà kutoa ushahidi wake, Bw. Valentine B. Chibwana, mlalamikaji, alieeleza Mahakama kama ifuatavyo:

Kwamba aliajiriwa na Chuo cha Ardhi tarehe 5/9/83, kama 'Senior Catering Officer', na kwamba alithibitishwa kazini mnamo tarehe 6/2/84. Kwamba mamlaka yake ya ajira ilikuwa ni Bodi ya Wakurugenzi, hakufahamu kuwa kulikuwa na mabadiliko kuhusu chombo chake cha ajira na nidhamu. Alipoona kuwa Idara aliyokuwa anafanya kazi haina mwelekeo, aliomba likizo isiyo na malipo ya siku 56, kuanzia tarehe 4/11/94, ambayo ingemalizika tarehe 29/12/94. Alijibiwa kukubaliwa likizo hiyo. Bw. Chibwana alitoa na kupokelewa Mahakamani barua ya ajira, barua ya uthibitisho kazini, barua ya maombi ya likizo-na barua ya kukubali likizo hiyo kama vielelezo — P. 1 hadi 4 kwa mpangilio huo.

Alipomaliza likizo yake isiyo na malipo, aliambiwa kuwa aende kufanya kazi upande wa Mabweni, kwa sababu sehemu ya Mgahawa ambako alikuwa anafanya kazi kulikuwa kumefungwa. Alipopata barua hiyo kielelezo P. 5, aliomba "Management" wamuachishe kazi kwa utaratibu wa watu wanaokosa kazi za kufanya, na apunguzwe kazi. Maombi hayo aliyafanya kwa maandishi. Hakupata jibu na Management, Mnaho tarehe 30/1/95, alijaziwa Karatasi No. 1 Chini ya Sheria ya Usalama Kazini, kwa kosa la kutokuripoti kazini. Alipopata form No. 1 alikwenda kwenye tawi la OTTU la Chuo cha Ardhi. Tawi la OTTU lilijaza Form No. 3 na kupeleka kwenye "Management" ya Chuo cha Ardhi na ndipo akaandikiwa barua ya kuachishwa kazi, Kielelezo P.8 Kwamba hakuitwa kujitetea katika kikao cha Tawi la Management, na hivyo alilazimika kukata rufaa kwa Katibu wa RAAWU Kanda ya Mashariki. Katibu wa RAAWU Kanda ya Mashariki aliunga mkono uamuzi wa "Management", kwa kuwa hakuridhika na uamuzi wa Katibu wa RAAWU Kanda ya Mashariki, alikata rufaa kwa Katibu wa RAAWU taifa. Bw. Chibwana ameeleza zaidi kuwa hakuridhika na hatua ya "Management" ya kumpangia kazi nje ya taaluma yake, kwa hali hiyo "Management" haikumtendea haki. Vile vile alimnyima nafasi ya kuteteta katika chombo kilichomuadhibu. Aliomba Mahakama itengue uamuzi wa kumuachisha kazi na iamuru kwamba arudishwe kazini ili maamuzi ya haki yafanyike.

Baada ya mlalamikaji kumaliza kutoa ushahidi wake, upande wa utetezi uliowakilishwa na Bw. Mtatula ulipewa nafasi ya kumhoji Bw. Chibwana ambaye katika kuhojiwa aliieleza Mahakama kuwa: Baada ya kumaliza likizo yake bila malipo aliripoti kazini tarehe 2/1/95. Aliporipoti Kazini, alimwendea Afisa Utumishi Mwandamizi kупинга kitendo cha kumpangia kufanya kazi Mabwenini. Aliomba tena likizo hiyo ya nyongeza bila malipo, na alikataliwa. Alipokataliwa likizo hiyo ya nyongeza bila malipo, alikaa tu nyumbani. Hakumbuki kama kulikuwa na masharti ya likizo yake bila malipo. Barua ya kumhamishia mabwenini haikueleza kazi gani ambayo angekwenda kuifanya. Aliwahi kuomba mkopo ili aweze kulipa ada ya watoto wake. Form No. 1 ilikuwa ni kusudio la kumfukuza kazi. Hakupata taarifa kuwa alikuwa anahitajika kwenye kikao cha RAAWU tawi na Management. Huo ukawa ndiyo mwisho wa mahojiano na mwisho wa ushahidi wa mlalamikaji.

Upande wa utetezi/ mlalamikiwa ultakiwa na Mahakama kuleta ushahidi wao wa utetezi na ulimwita Bw. Ayub Mbega, kuwa shahidi wa kwanza. Hata hivyo baada ya ushahidi wa Bw. Mbega kusikilizwa Mahakama ilitoa Amri kama ifuatavyo:

"Mahakama: Kutokana na Madai ya mwakilishi wa walalamikiwa Bw. Mtatula kuwa hakuwa anafahamu utaratibu, na kwamba ye ye alitaka pia kutoa ushahidi wa upande wa utetezi, unaanza upya, kwa kuwa Bw. Matula alipata wasaa wa kuusikiliza ushahidi wa Bw. Mbega (DW. 1), ushahidi huo pia unaufutwa.

Kutokana na Amri hiyo ya Mahakama ushahidi wa Bw. Mbega (DW. 1) umefutwa, hivyo hauna haja ya kuanisha kwa kuwa hautatumika kabisa katika kufikia uamuza wa shauri hili. Shahidi wa pili (D ". 2) wa upande wa utetezi ni Bw. HALFANI MTATULA ambaye aliieleza Mahakama kama ifatavyo:

Kwamba ye ye aliajiriwa na chuo cha ardhi mnamo tarehe 31/1/81 kama Afisa Utumishi. Anamfahamu mlalamikaji ambaye alikuwa amejiriwa na chuo kama 'Senior Catering Officer' tarehe 5/9/1983, na kwamba aliendelea na wadhifa huo hadi alipoachishwa kazi mnamo tarehe 2/1/1995. mlalamikaji alikuwa anafanya kazi katika Idara ya Mshauri wa wanafunzi kitengo cha 'Caterer' ya wanafunzi na 'Canteen' ya Wafanyakazi, na kwamba alikuwa chini ya Mshauri wa Wanafunzi. Mlalamikaji aliomba likizo ya siku 56 bila malipo. Likizo hiyo aliruhusiwa na kwamba alianza tarehe 4/11/1994 na ilimalizika tarehe 29/12/1994. Kwa kuwa kulikuwa na mapumziko kitaifa ya siku 3 mfululizo mlalamikaji alitakiwa kurejea kazini tarehe 2/1/1995. kabla ya likizo hiyo ya siku 56 kumalizika, mlalamikaji aliomba likizo nyingine ya miezi sita (Kielelezo D.1 na D.2 vyahusika). Katika barua ya kumkubalia likizo ya siku 56, mlalamikaji aliambiwa wazi kuwa hataruhusiwa kuongeza likizo nyingine. Uongozi wa chuo ulimkatalia maombi yake ya nyongeza ya likizoya miezi sita, (kielelezo D.4) kwa barua ya tarehe 6/1/95. Siku hiyo

hiyo ya tarehe 6/1/95, Mlalamikaji aliandikiwa barua nyingine ya kumtaka aripoti kazini kwa Mkuu wake wa Idara, ambaye ni Mshauri wa wanafunzi (Kielelezo D.5). Mlalamikaji hakuripoti kazini. Hata hivyo mlalamikaji aliandikiwa barua nyingine mnamo tarehe 19/1/95 ikimtaka aripoti kazini ifikapo tarehe 24/1/95 saa 1½ asubuhi. (Kielelezo D. 6 chahusika). Alipopata barua hiyo mlalamikaji alijibu kwa barua ya tarehe 23/1/95, kwamba asingeweza kufika kazini kwa sababu alikuwa anafanya kazi kwa mtu aliyemkopsha fedha za kusomesha watoto wake. (Kielelezo D. 7 chahusika). Mnamo tarehe 30/1/95, mlalamikaji alijaziwa form No. 1 chini ya Sheria ya Usalama Kazini kwa kosa la kutohudhuria kazini. Mlalamikaji alikataa kupokea fomu hiyo Na. 1 na mnamo tarehe 6/2/95, mlalamikaji alipelekewa tena fomu Na. 1 ambayo vile vile alikataa kuipokea (Kielelezo D.8). Mhudumu aliyepeleka form hiyo aliandika barua kwa uongozi wa chuo kuhusu jambo hili. Baada ya uongozi wa chuo kuona kwamba mlalamikaji amekataa kupokea form No. 1, uongozi wa chuo uliandika barua kwa Mwenyekiti wa OTTU Mahala pa kazi, na Mwenyekiti wa OTTU alipokea form hiyo No.1 na kumkabidhi mlalamikaji, ambaye aliipokea mnamo tarehe 13/2/95. Mwenyekiti wa OTTU alijaza Form No. 2 na kuomba uongozi wa chuo kukutana na Tawi la OTTU kuzungumzia suala la mlalamikaji (Kielelezo D.10). Mnamo tarehe 24/2/95, uongozi wa chuo ulimjibu Mwenyekiti wa OTTU Tawi la chuo ukimfahamisha kuwa mkutano ufanyike tarehe 28/2/95 (Kielelezo D.11). Mnamo tarehe 28/2/95 uongozi wa Tawi la OTTU la chuo cha Ardhi ulikutana kama ilivyopangwa na kikao kiliona kuwa mlalamikaji ana makosa na ilipendekezwa kuwa afukuzwe kazi. Baada ya kikao hicho mwenyekiti wa Tawi alijaza form No.3, ambapo Tawi liliomba kuwa mlalamikaji aachishwe kazi. Uongozi wa chuo ulikubali maombi hayo na hatimaye kikao cha Kamati ya Ajira na Maendeleo ya Wafanyakazi kilichokaa tarehe 12/6/95, baada ya kujadili kwa kina suala la Bw. Chibwana kilikubali maombi ya Mwenyekiti wa OTTU kwamba Bw. Valentine Chibwana aachishwe kazi mara moja na alipwe haki zake zote kwa kufuata Kanuni na Sheria zilizopo (Miniti za kikao kielelezo D.13 - chahusika). Mnamo tarehe 14/6/95 mlalamikaji aliandikiwa barua ya kumwachisha kazi (Kielelezo D.14). Tarehe 22/6/95 mlalamikaji aliandika barua kwa uongozi kutaka kufahamishwa mafao yake (Kielelezo D.1). Mlalamikaji alilipwa haki zake zote na alizipokea. Hata hivyo, hatimaye uongozi wa chuo ulipata taarifa kuwa mlalamikaji alikuwa amejiariwa na Shirika la Reli, barua yenye Kumb. Na. ARIC/TW.1/01 inathibitisha hivyo (kielelezo D. 19). Huo ukawa ndiyo mwisho wa ushahidi wa shahidi wa pili Bwana Mtatula.

Baada ya ushahidi huu, Bwana Ngulla mwakilishi wa mlalamikaji alipewa nafasi ya kumhoji shahidi wa pili wa utetezi na katika mahojiano, shahidi huyu alieleza kuwa; ye ye alihitimu Civil Service Training Centre baadaye alikwenda kusomea mambo ya utawa huko Uingereza. Kwamba mlalamikaji aliajiriwa kama "Senior Catering Officer". Kwamba walimwandikia mlalamikaji Karatasi Na. 1.

Baada ya mahojiano baina ya Bwana Ngulla na shahidi wa pili kufanyika kama ilivyoonyeshwa hapo juu ndipo Bwana Ngulla alitoa hoja ya kuwa Mheshimiwa Naibu Mwenyekiti Mlelwa alikuwa na upendeleo, hivyo akaomba shauri hili lipangwe kwa Mwenyekiti au Naibu Mwenyekiti mwingine kuendelea nalo.

Kama ambavyo nimekwishaeza hapo awali, nilipangiwa kuendelea kusikiliza shauri hili. Pande zote mbili zilikubali tuendelee kusikiliza ushahidi wa shahidi watatu upande wa utetezi.

Shahidi wa tatu alikuwa ni Bwana Justine Maingi, ambaye baada ya kuapishwa, alieleza Mahakama kama ifuatavyo:

Kwamba yeche ni Mwenyekiti wa Tawi la RAAWU Chuo cha Ardhi. Kama mwajiriwa wa chuo, yeche ni Afisa Ugavi Mwandamizi. Anamfahamu mlalamikaji Bwana Chibwana kama mfanyakazi na mwanachama wa RAAWU. Anakumbuka kuwa Bwana Chibwana aliwahi kuomba likizo bila malipo ya siku 56 mwaka 1994. Kwamba Bwana Chibwana alikuwa ni "Senior Catering Officer" katika "Canteen" ya chuo. Baada ya likizo hiyo ya siku 56 kumalizika, Bwana Chibwana aliomba likizo ya miezi 6 bila malipo ambayo alikataliwa, na Bwana Chibwana hakurudi kazini. Aliandikiwa Fomu Na. 1 ambayo ni kusudio la kumfukuza kazi. Kama Mwenyekiti wa RAAWU alipewa nakala na kuombwa ampelekéé tarehe 13/2/95. Shahidi alikiri kujaza fomu Na. 2 kupinga kusudio la mwajiri la kumfukuza kazi Bwana Chibwana. Sababu za kupinga kusudio hilo ni kuwa hakuwa na sababu za kumfukuza kazi Bwana Chibwana kwa kuwa "canteen" ilikuwa imefungwa. Tarehe 28/2/95 Tawi pamoja na "Management" walikutana kuzungumzia suala hilo na kwamba mlalamikaji hakuwepo, pengine aliona kuwa Tawi litamsimamia. Bwana Mdingi alieleza zaidi kuwa yeche alikuwa anamtetea kama mwanachama wake. Anaelewa kuwa mtu akiwa nje ya kazi kwa muda siku 4 anakuwa amejifukuzisha kazi. Sehemu ambayo Bwana Chibwana alikuwa amehamishiwa hapakuwa na fani yake akiwa kama mpishi. Bwana Chibwana hakuwahi kuripoti katika sehemu aliopangiwa kufanya kazi. Kwamba katika kikao cha tarehe 28/2/95 ilikubalika kuwa kwa kutokuwepo kazini Bwana Chibwana kwa zaidi ya siku 4 alipashwa kufukuzwa kazi. Baada ya hapo Bwana Mdingi anasema alijaza fomu Na.3 kuomba Menejimenti imwachishe kazi badala ya kumfukuza. Katika kikao cha Kamati ya Ajira na nidhamu ambayo ilikaa tarehe 12/6/95, pamoja na mambo mengine kujadili suala la Bwana Chibwana Bwana Mdingi alialikwa kama mjambe. Wajumbe wote wa Kamati walisema sheria itekelezwe, hata hivyo yeche alimuombea Bwana Chibwana ahurumiwe na Kamati ilikubali kwamba Bwana Chibwana aachishwe kazi badala ya kufukuzwa. Bwana Chibwana aliandikiwa barua ya kuachishwa kazi tarehe 14/6/95 ikimfahamisha kuwa alikuwa ameachishwa kazi kuanzia tarehe 2/1/95. Kwamba, Bwana Chibwana aliandika barua kutaka kujua malipo yake anayostahili. Kwamba Bwana Chibwana alitendwa haki katika kuachishwa kazi.

Baada ya ushahidi huo Bwana Ngulla mwakilishi wa mlalamikaji alipata nafasi ya kumuhoji Bwana Mdingi, ambaye katika mahojiano hayo Bwana Mdingi alieleza kuwa; amewahi

kusikia kuhusu haki ya misingi ya asili. Kwamba Bwana Chibwana alipewa taarifa ya kuhudhuria kikao kati ya Menejimenti na RAAWU lakini hakutaka. Bwana Mdingi alieleza kuwa yeche mwenyewe ndiye aliymfahamisha Bwana Chibwana kuhusu kikao hicho cha tarehe 28/2/95. Katika kikao cha nidhamu na ajira cha tarehe 12/6/95 hafahamu kama Bwana Chibwana aliitwa. Kwamba kikao kilitoa uamuzi wa haki wa kumwachisha kazi Bwana Chibwana badala ya kumfukuza. Mamlaka ya Ajira ya Bwana Chibwana ni Kamati ya Ajira na Nidhamu. Kwamba haikuwa ni mara ya kwanza kwa Bwana Chibwana kujadiliwa na Kamati ya Nidhamu na Ajira. Baada ya mahojiano hayo huo ukawa ndiyo mwisho wa ushahidi kwa upande wa utetezi.

Pande zote mbili zinazohusika na mgogoro huu wa uchunguzi zilitakiwa kuwasilisha hoja zao za mwisho kwa maandishi na zilifanya hivyo.

Shauri hili lilipoanza kusikilizwa walikuwepo washauri ambaa ni Bwana P. Jonathan kutoka - OTTU/TUICO na Bwana Kaberege kutoka - ATE. Washauri hawa baada ya shauri hili kumalizika kusikilizwa hawakuwahi kutoa maoni yao. Bwana Kaberege ilifahamika kuwa alikwisha staafu kazi, hivyo hangeweza kusatikana kutoa maoni yake. Bwana Jonathan ilifahamika kuwa alikuwa safarini. Hata hivyo sheria ya Mahakama ya Kazi katika fungu la 19(3) la Sheria Na. 3 ya mwaka 1990 linatoa Mamlaka kwa Mahakama kuendelea kutoa uamuzi bila kuwapo kwa maoni ya Washauri kutokana na sababu moja au nyingine. Kwa hali hiyo, ni wajibu wangu sasa kulitolea shauri hili uamuzi.

Nimeupitia kwa makini ushahidi wa mlalamikaji kama nilivyouanisha hapo juu, pamoja na ushahidi wa utetezi wa shahidi wa pili na watatu. Kama nilivyouanisha eleza hapo awali hapakuwepo na sababu ya kuainisha ushahidi wa shahidi wa kwanza wa utetezi kwa sababu ulikuwa umefutwa na Mahakama, na hivyo haungeweza kutumika kufikia uamuzi wa shauri hili. Nimepitia kwa makini vile vile hoja za wawakilishi wa pande zote mbili na kuzitilia maanani.

Ili kufikia uamuzi wa shauri hili ni vizuri kuangalia kama hoja alizowasilisha Kamishna wa Kazi ili kufanyiwa uchunguzi zimejibiwa katika ushahidi uliotolewa na pande zote mbili. Hoja hizo ni zifuatazo:

- Kama uongozi wa chuo ulifuata sheria ya kumwachisha kazi Bwana V. Chibwana
- Kama hatua za kuwachisha kazi Ndugu V. Chibwana zilikuwa ni za haki kwa mujibu wa sheria za utovu wa nidhamu.
- Kama kitendo cha Menejimenti cha kubadilisha Mkataba wa Ajira ulikuwa ni halali kwa mujibu wa Sheria za kazi.
- Kama sheria nyingine zinazoambatana na mahusiano kazini zilifuatwa.

Hoja ya kwanza na ya pili (a) na (b) hapo juu zinazoshabihiana hivyo zitajibiwa kwa pamoja.

Kutokana na ushahidi wa pande zote mbili haipingwi kwamba mlalamikaji alikuwa amejiriwa na Chuo cha Ardhi kama "Senior Catering Officer". Vile vile kwamba mnamo tarehe 4/11/94 mlalamikaji aliomba likizo isiyi na malipo ya siku 56, ambayo ingemalizika tarehe 29/12/94, na alipewa. Ushahidi unaonyesha zaidi kwamba mlalamikaji alipashwa kurudi kazini kuanzia tarehe 2/1/95 kwa sababu ya mapumziko ya kiserikali ya siku tatu katika tarehe 29/12/94 hadi tarehe 2/1/95. Kwamba kabla ya siku 56 kwisha, mlalamikaji aliomba likizo bila malipo ya miezi 6 na akakataliwa, hivyo alipashwa kurudi kazini. Mlalamikaji amekiri katika ushahidi wake alipohojiwa na mwakilishi wa utawala /mdaiwa Bwana Mtatula, kwamba baada ya kukataliwa likizo ya nyongeza bila malipo, aliamua kukaa tu nyumbani. Mlalamikaji hakurudi kazini hata baada ya kuarifiwa kwa barua ya tarehe 6/1/95 na barua ya tarehe 19/1/95 ikimtaka arudi kazini ifikapo tarehe 24/1/95 saa 1½ asubuhi.

(Vielelezo D. 5 na D.6). Kwa ushahidi mwiningine wa mlalamikaji mwenyewe, baada ya kupata barua ya tarehe 19/1/95 ya kumtaka aripoti kazini, yeze aliandika barua mnamo tarehe 23/1/95 akieleza kwamba asingeweza kufika kazini kwa sababu alikuwa anafanya kazi kwa mtu aliyemkopesha fedha ya kusomesha watoto wake (kielelezo D. 7). Ni vizuri kunukuu sehemu ya barua hiyo ili kujua hasa mlalamikaji amesema nini:

"Valentine B. Chibwana,
c/o Chuo cha Ardhi,
S.L.P. 35176,
Dar es Salaam.
23/01/1995

Mkuu wa Chuo,
Chuo cha Ardhi,
S.L.P. 35176,
DAR ES SALAAM.

YAH: LIKIZO BILA MALIPO

Kwa misingi hiyo azma yako ya kunitaka nifike kazini tarehe 24/1/95 sitaitekeleza, kwa vile nijuavyo mimi nikawa niliruhusiwa niendeleee na likizo bila malipo katika kutekeleza masharti ya mtu aliyenipatia fedha za kuwasomesha watoto wangu baada ya chuo kunieleza kuwa hakina fedha ya kunipatia (kwa shughuli hiyo

Wako mtiifu,

Sgd:

V. B. CHIBWANA"

(Msisitizo katika nukuu hiyo ya barua ni wangu).

Kwa ushahidi wake mwenyewe alioutoa Mahakamani wakati anahojiwa kwa kusema kuwa baada ya kukataliwa nyongeza ya likizo ya miezi 6, aliamua kukaa tu nyumbani, na kwa ushahidi wa maandishi kielelezo D. 7 kama ambavyo nimeinukuu barua yake hapo juu, ni dhahiri kwamba

mlalamikaji kwa kukataa kuripoti kazini amekiuka fasili "K" ya fungu la 19 na fungu la 20 la Sheria ya Usalama Kazini Na. 62 ya mwaka 1964 - Sura ya 574.

Kwa mlalamikaji kukiuka sheria hiyo mwajiri alipashwa kufanya nini? Mwajiri alitumia taratibu za kisheria kwa kumpatia mlalamikaji Fomu Na. 1 kuitia kwa Mwenyekiti wake wa Chama cha Wafanyakazi. Mwenyekiti wake wa Chama cha Wafanyakazi. Mwenyekiti wa RAAWU aliomba kikao kifanyike baina ya uongozi wa chuo na Tawi la RAAWU kwa kujaza Fomu Na. 2, (Kielelezo D. 10) Mwenyekiti wa RAAWU alikuwa shahidi wa tatu wa upande wa utetezi ambaye alikiri kumpa mlalamikaji taarifa ya kikao baina ya uongozi na Tawi kilichofanyika tarehe 28/2/95, hata hivyo mlalamikaji hakuhudhuria kikao hicho. Mwenyekiti wa RAAWU ambaye ndiye mtetezi wa mlalamikaji akiwa mwanachama wake wakati huo, katika ushahidi wake anakiri kwamba mlalamikaji alitenda kosa kwa kutohudhuria kazini zaidi ya siku 4 baada ya kutakiwa aripoti kazini. Kwa kujua kosa la mwanachama wake Mwenyekiti wa RAAWU baada ya kikao cha uongozi na Tawi la Wafanyakazi alijaza Fomu Na. 3, akimuombea mwanachama wake ili apunguziwe adhabu. Aliomba aachishwe kazi badala ya kufukuzwa. Mlalamikaji alifahamishwa kosa lake, Chama cha Wafanyakazi RAAWU, kilimtaka afike kwenye kikao baina ya uongozi na Tawi lakini hakufika. Hata hivyo Chama cha RAAWU kikisimamiwa na Mwenyekiti kilimtetea kwa nguvu zote. Mlalamikaji alipewa nafasi ya kujitetea akaipuuza hata hivyo alitetewa na tawi lake la Chama. Haiwezi ikaelezeka kwamba mlalamikaji hakupewa nafasi ya kujitetea. Utetezi uliofanywa na Mwakilishi wa mlalamikaji ulipelekwa kwenye kikao cha Kamati ya Nidhamu na Ajira cha tarehe 12/6/95, na Bwana Mdigi mwakilishi wa mlalamikaji aliitwa katika kikao hicho na aliendeleza utetezi wake kwa kumwombea mlalamikaji kuwa apunguziwe adhabu na kwamba aachishwe kazi badala ya kufukuzwa na utetezi huo ulikubaliwa. Hata katika kikao cha Kamati ya Nidhamu na Ajira, mlalamikaji alisikilizwa kuptita mwakilishi wake. Kwa hali hiyo hakuna misingi ya asili ya haki za mlalamikaji ambayo ilikiukwa.

Licha ya hayo niliyoyaeleza hapo juu ushahidi wa mlalamikaji mwenyewe kuitia kielelezo D. 7, unaonyesha dhahiri kwamba mlalamikaji ndiye aliyesitisha ajira yake na mwajiri wake Chuo cha Ardhi. Ushahidi huu upo katika barua ambayo nimekwisha inukuu hapo juu. Siyo vibaya kurudia nukuu hiyo:

"..... Kwa misingi hiyo azma yako ya kunitaka nifike kazini tarehe 24/1/95 sitaitekeleza, kwa vile nijuavyo mimi ni kuwa niliruhusiwa niendeleee na likizo yangu bila malipo katika kutekeleza masharti ya mtu aliyenipatia fedha za kuwasomesha watoto wangu baada ya chuo kunieleza kuwa hakina fedha ya kunipatia kwa shughuli hiyo".

Sehemu ya barua hiyo haiwezi kuelezeza vinginevyo isipokuwa kwamba; kwanza mlalamikaji amekataa kurudi kazini tarehe 24/1/95; kwa maneno ".... azma yako ya kunitaka nifike kazini tarehe 24/1/95, sitaitekeleza". Pili inaonyesha kwamba mlalamikaji amepata ajira sehemu nyingine mbali ya ajira ya mwajiri wake. Hii imedhihirishwa

na maneno: " *katika kutekeleza masharti ya mitu aliyenipatia fedha za kuwasomesha watoto wangu baada ya chuo kunieleza kuwa hakina fedha kwa shughuli hiyo*"

Kwa misingi hiyo mlalamikaji alikwisha kujiachisha kazi yeze mwenyewe kabla ya kuachishwa kwa utaratibu uliotumika. Kutokana na hayo yote niliyokwisha yaeleza hapo juu ni uamuzi wangu kuwa, uongozi wa chuo ulifuata sheria ya kumwachisha kazi Bwana Valentine Chibwana. Vile vile kwamba hatua za kumuachisha kazi zilikuwa za haki kwa mujibu wa sheria za utovu wa nidhamu.

Hoja ya kwamba Menejimenti ilibadilisha Mkataba wa Ajira, hakuna ushahidi kama huo uliotolewa katika Mahakama hii. Mlalamikaji kwa kuambiwa akaripoti kwa Mkuu wa Idara ambayo ipo chini ya Mshauri wa Wanafunzi siyo kubadili Mkataba wa Ajira. Kubadili mkataba wa Ajira ni kuanza kwa ajira impya, ikiwa ni pamoja na Mshahara, Masharti mapya na marupurupu yake. Inasemekana tu kwamba mlalamikaji alihamishiwa sehemu ya Mabweni ya Wanafunzi kwa sababu "Canteen" yeze akiwa" Senior Catering Officer" ilikuwa imefungwa. Huu ni uhamisho wa kawaida kwa Kiidara. Mlalamikaji alikuwa hajari poti kazini kwa hiyo hakujua kuwa angepewa wadhifa gani katika Idara hiyo. Kwa hali hiyo haiwezi kuelezeza kwamba Menejimenti kwa kumpa mlalamikaji uhamisho wa Kiidara imebadilisha Mkataba wa ajira.

Hoja ya nne ya Kamishna wa Kazi, kuhusu kama sheria nyingine zinazoambatana na mahusiano kazini zilifuatwa, imejibiwa Sheria zinazohusika ni misingi ya asili ya haki za mlalamikaji ambayo nimekwisha sera kwamba haikukiukwa, kwa sababu ijapo kuwa mlalamikaji alifahamishwa kosa lake na baadaye kuitwa kwenye kikao cha Menejimenti na Tawi la RAAWU, hakwenda hivyo kujinyima yeze mwenyewe haki ya kusikilizwa. Hata hivyo mlalamikaji alisikilizwa kwa kuwakilishwa na Mwenyekiti wake wa RAAWU na akatetewa hadi kwenye kikao cha Kamati ya nidhamu na Ajira ambacho kilikubali kumpunguzia adhabu. Sheria nyingine ni Sheria ya Usalama Kazini ambayo ilifuatwa baada ya Mlalamikaji kukiuka fasili "K" ya fungu la 19 na 20 ya Sheria Na. 62 ya mwaka 1964 - Sura 574. Mwisho Mlalamikaji ndiye aliye katisha ajira yake kwa kukataa kurudi/kuripoti kazini kama niliyokwisha eleza hapo awali, na kwamba alitafuta ajira nyingine na kuajiriwa kama niliyofafanua Kielelezo D. 7 hapo juu.

Kutokana na hayo yote niliyokwisha yaeleza hapo juu ni uamuzi wangu kwamba mlalamikaji ya mlalamikaji katika Mgogoro huu wa Uchunguzi hayana msingi na ninayatupilia mbali. Mlalamikaji aliajishwa kazi kihalali kwa mujibu wa sheria na taratibu za kazi kwa utovu wa nidhamu. Uamuzi huu umetolewa leo tarehe 21 mwezi wa 12 mwaka 1999 na unakuwa TUZO ya Mahakama yenyeye nguvu za kisheria.

Sgd.

J. B. TENDWA,
Naibu Mwenyekiti

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 861

MGOGORO WA UCHUNGIZI NA. 8 YA 1998
baina ya

RAMADHANI M. MATIMBWA - DAR ES SALAAM
na

N.B.C. HOLDING CORPORATION DAR ES SALAAM
UAMUZI

Uamuzi katika Mgogoro huu wa Uchunguzi unatokana na pingamizi la awali, lililosilishwa na Wakili wa Utetezi Bibi Kashonda wakati shauri hili lilipokuja kwa ajili ya kusikilizwa minamo tarehe 20/10/98.

Katika kuwasilisha pingamizi la awali, Bibi Kashonda aliwasilisha hoja mbili na kuionomba Mahakama kutupilia mbali Mgogoro huu wa Uchunguzi. Hoja hizo ni:-

- (a) Mlalamiko ya Mlalamikaji yamewasilishwa nje ya muda,
- (b) Utaratibu wa kuwasilisha Mgogoro huu Mahakamani haukuatuwa.

Kwa kutetea hoja zake hizo Bibi Kashonda aliiezeza Mahakama kwamba; Mlalamikaji alipunguzwa kazi tarehe 1/5/94 na aliamua kuka kimya hadi tarehe 14/11/97 ambapo alipeleka malalamiko yake moja kwa moja kwa Kamishna wa Kazi kwa njia ya barua. Kufuatana na kifungu cha 4(1)(2) cha Sheria ya Mahakama ya Kazi Na.2 ya mwaka 1993 Mlalamikaji akiwa Mwanachama wa Chama cha Wafanyakazi OTTU/TUICO alipashwa kupeleka malalamiko yake kwa Tawi la Chama chake ndani ya siku 7, ambao wangetoa taarifa ya kuwapo Mgogoro katika siku 14. Kabla ya hapo angepashwa kujaziwa Fomu TD. 2 ambayo ni lazima Kisheria. Kwa hali hiyo Mgogoro huu haupo imbele ya Mahakama hii kisheria na unapashwa kutupiliwa mbali.

Kuhusu hoja ya pili ya pingamizi la awali, Bibi Kashonda aliiezeza Mahakama kwamba; Mlalamikaji alikuwa katika ngazi ya Uongozi, na hivyo kwa mujibu wa Sheria Na. 2 ya Mahakama ya Kazi ya mwaka 1993, Mlalamikaji alipashwa kuthibitishwa na Afisa Kazi kwamba yupo katika nafasi ya Uongozi chini ya fungu la 10 la Sheria Na. 2 ya mwaka 1993 kwa kujaziwa Fomu TD 1 na hivyo kumpa uwezo wa kuleta Mgogoro huu Mahakamani. Bibi Kashonda aliirejesha Mahakama katika kesi ya JUMA NKONDO Vs TOL (Tanzania Oxygen Ltd.) High Court Civil Case No. 239/94; ambapo Mh. Jaji Kyando alitupilia mbali shauri la Mlalamikaji hakuambatanisha Fomu ya Uthibitisho ya Afisa wa Kazi kuthibitisha kwamba Mlalamikaji alikuwa katika nafasi ya Uongozi, na hivyo amekiuka utaratibu. Vile vile Bibi Kashonda aliirejesha Mahakama katika Shauri la George Shambe Vs NASACO - TD. 25/93 ambapo Mheshimiwa Jaji Bahati alitupilia mbali Mgogoro huo wa Kikazi kwa kuwa Mlalamikaji hakufuata utaratibu wa Kisheria kama huo na kwamba malalamiko hayo yamefikishwa Mahakamani nje ya muda. Bibi Kashonda kwa kusisitiza hoja yake aliirejesha tena Mahakama hii katika Mgogoro wa Kikazi Na. 11 wa 1997 HAMISI UREMBO Vs ALUMINIUM AFRICA Ltd. ambapo Mahakama ilitupilia mbali Mgogoro wa Walalamikaji kwa kuwa utaratibu wa kuwasilisha Mgogoro huo katika Mahakama hii haukuatuwa.

Certified true copy of the original.

B. E. NYAMUBI,
Registrar

Bibi Kashonda alilalamika kuwa Shauri hili lilkwisha amuliwa katika kesi ya madai Na. 336/94 katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, ambapo madai ya Mlalamikaji na wenzake dhidi ya NBC yalitupiliwa mbali. Madai hayo katika Mahakama ya Kisutu ni sawa na madai yaliyopo katika Mahakama hii. Kutohama na fungu la 9 la Civic Procedure Code ashauri hili limekwisha amuliwa na hivyo Sheria inakataza madai kama haya kufikishwa tena Mahakamani. Vile vile Mlalamikaji na Wenzake baada ya shauri lao kutupiliwa mbali na Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, walifungua shauri lingine Mahakama Kuu likiwa ni Shauri la Madai Na. 112/98. Bibi Kashonda ameiomba Mahakama ifute Mgogoro huu na kuona kwamba Mlalamikaji anatumia Mahakama kufungua madai yale yale tama anavyotaka.

Kwa misingi hiyo Bibi Kashonda ameiomba Mahakama kutupilia mbali madai ya Mlalamikaji kwa kuwa hayana msingi Kisheria.

Mlalamikaji alipewa nafasi ya kujibu hoja ya pingamizi fa awali kama ilivyowasilishwa na Bibi Kashonda Wakili wa Mlalamikiwa NBC Holding Corporation. Bw. Ramadhani Matimbwa alijibu hoja hiyo kwa kuieleza Mahakama kwamba;

Shauri hili limeletwa katika Mahakama hii na Kamishna wa Kazi kwa mujibu wa fungu la 9(a) la Sheria ya Mahakama ya Kazi Na. 2 ya mwaka 1993. Katika kifungu hicho cha Sheria hakuna muda maalumu wa kuwasilisha Mgogoro Mahakamani na Kamishna wa Kazi. Endapo Afisa wa Kazi hakutoa maoni yake kuhusu wadhifa au ngazi ya Utumishi ya Mlalamikaji basi shauri linaweza kusitishwa ili kumpa nafasi Afisa wa Kazi kufanya hivyo. Bw. Matimbwa aliirejesha Mahakama katika Shauri la GOSBERT EDWARD RWEYEMAMU Vs TWICO Civic Case No. 73/91. Kwamba, kwa misingi hiyo Shauri hili linapashwa kusitishwa hadi maoni ya Afisa wa Kazi yapatikane. Kuhusu shauri la madai Mahakama ya Kisutu ni kwamba lilifutwa kwa kuwa Mahakama hiyo haikuwa na namlaka (Jurisdiction).

Kamishna wa Kazi anaweza kuleta Shauri lolote chini ya fungu la 8(a) la Sheria Na. 2 ya 1993, katika Mahakama hii. Kuhusu shauri la madai Na. 112/98 Bw. Matimbwa amedai kuwa yeye halimhusu kwa kuwa yeye bado hajalipa fedha kwa Wakili.

Alimaliza kwa kuionba Mahakama kutupilia mbali pingamizi la awali. Katika kusikiliza shauri hili kwenye hoja ya pingamizi la awali, nilisaidiwa na Washauri Bw. H. Ngwo kutoka OTTU/TUICO na Bw. Mwanyika kutoka ATE (Association of Tanzania Employers). Niliwataka wanipe maoni yao kuhusu pingamizi hili la awali kama ambavyo nimeelezea pande zote mbili hapo juu. Washauri walishauri kwamba;

Mgogoro uliopo mbele ya Mahakama ya Kazi umeletwa nje ya muda unaoruhusiwa kisheria. Aidha Mlalamikaji kufungua na kuendesha kesi zenyenye madai yanayofanana Mahakama Kuu na Mahakama ya Kazi kwa wakati immoja siyo sahihi, na isitoshe madai kama hayo yalikwishatupwa (dismissed) na Mahakama ya Kisutu. Mahakama ya Kazi kuendelea kusikiliza shauri ambalo liko Mahakama Kuu si

halali Kisheria. Vile vile Mlalamikaji hakuchukua hatua zinazostahili kisheria kuuleta Mgogoro huu katika Mahakama ya Kazi kwa mujibu wa Sheria.

Baada ya kupata maoni ya Washauri ni wajibu wangu sasa kulitolea Uamuzi shauri hili.

Bila kupoteza muda, maelezo ya pingamizi la awali yaliyotolewa na Wakili wa Utetezi Bibi Kashonda ni sahihi, kwamba Mgogoro huu wa Uchunguzi haupo mbele ya Mahakama hii kisheria, kwanza kwa kutokidhi haja ya matakwa ya Sheria ya Mahakama ya Kazi Na. 3 ya mwaka 1990, kama ilivyorekebishiwa na Sheria Na. 2 ya mwaka 1993. Mara tu Mlalamikaji alipoona kwamba hakuridhika na Uamuzi wa kumuachisha kazi alipashwa kuchukua hatua za haraka kuanzisha Mgogoro chini ya kifungu cha 4(1)(2) cha Sheria Na. 3 ya Mahakama ya Kazi ya mwaka 1990, kama ilivyorekebishiwa na Sheria Na. 2 ya 1993, pamoja na fungu la 10 la Sheria hiyo la kumtaka Afisa wa Kazi kutoa hati ya uthibitisho kwamba Mlalamikaji yuko katika nafasi ya Uongozi hivyo kupata mamlaka ya kuwasilisha Mgogoro huu katika Mahakama ya kazi. Ninakubaliana na hoja ya Bibi Kashonda.

Ingawa Kamishna wa Kazi anayo mamlaka ya kuwasilisha Mgogoro wa Uchunguzi chini ya fungu la 8(a) la Sheria Na. 2 ya mwaka 1993, hata hivyo mamlaka haya hayawesi kutumiwa na Mlalamikaji wakati wowote hasa Mlalamikaji anapopashwa kutekeleza wajibu wake kisheria kwa wakati uliopangwa na akapuza kufanya hivyo. Mlalamikaji alichagua kutumia Mahakama nydingine kutafuta haki yake na akaacha kufuata utaratibu aliopashwa kufuata kwa mujibu wa Sheria ya Mahakama ya Kazi na hivyo kumfanya akiuke utaratibu wa Kisheria. Miaka mitatu baada ya kupita wakati wa kufuata utaratibu wa Sheria ya Mahakama ya Kazi ndipo akaamua kupeleka malalamiko yake kwa Kamishna wa Kazi. Kufanya hivi ni kumtumia Kamishna kama Punda ili aufikishe mzigo wake. Vile vile Mlalamikaji ameamua kupeleka-malalamiko au madai yake katika Mahakama Kuu ambapo shauri hilo bado ambapo shauri hili bado halijashughulikiwa. Mahakama hii haiwezi kukubali kuyumbishwa au kuruhusu vyombo vyaya utoaji maoni ya Washauri wa Mahakama hii pamoja na Wakili Bibi Kashonda mtoya hoja ya pingamizi la Awali kwamba; Mgogoro huu wa Uchunguzi haupo mbele ya Mahakama hii kihalali kwa kukiukwa utaratibu wa kisheria na pili kwamba umepitwa na wakati; hivyo basi Mahakama hii haina mamlaka na wajibu wa kusikiliza Mgogoro huu wa Uchunguzi. Mgogoro huu ninautupilia mbali na Uamuzi huu unakuwa ni TUZO ya Mahakama.

Uamuzi huu umetolewa leo tarehe 17/11/98 na kuwekwa sahihi yangu.

sgd.
J. B. TENDWA
Naibu Mwenyekiti

Certified true copy of the original.

B. E. NYAMUBI,
Registrar

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 862

UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI

(Katika Mahakama Kuu ya Tanzania, Dar es Salaam)

SHAURI NAMBAJI 52 YA MWAKA 2000

Col. Rashid R. Kizoka, Marehemu
na

Sindano Rashid Kizoka, Muombaji

TAARIFA YA KAWAIDA

(Kanuni ya 75)

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika Mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inasaa kabla ya kutolewa kwa barua za usimamizi wa Mirathi kwa muombaji aliyetajwa hapo juu/kwa waombaji walijotajwa hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnaimo au kabla ya tarehe 23 mwezi wa Januari mwaka wa 2001.

Imewasilishwa Dar es Salaam leo tarehe 2 mwezi wa Novemba mwaka 2000.

Naibu Msajili

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 863

DEED POLL

BY THIS DEED, and pursuant to DECREE FOR DIVORCE granted on 22nd day of September, 2000, I, the undersigned NTUMIGWA MOSSES MWAMPOONDELE, formerly known as NTUMIGWA MOSSES MWAKISOPILE of P.O. Box 9191, Dar es Salaam, do hereby absolutely renounce and abandon the use of the said name of NTUMIGWA MOSSES MWAKISOPILE and in lieu thereof do assume the name of NTUMIGWA MOSSES MWAMPOONDELE. In pursuance of such change of name of aforesaid I hereby declare that I will be known at all times hereafter in all records, deeds and instruments in writing and in all actions and proceedings in all dealings and transactions and upon all occasions whatsoever and sign the said name of NTUMIGWA MOSSES MWAMPOONDELE as my name in lieu of the former name of NTUMIGWA MOSSES MWAKISOPILE renounced as aforesaid. And I do hereby authorise and request all persons to designate, describe and address me by such name of NTUMIGWA MOSSES MWAMPOONDELE.

IN WITNESS WHEREOF the deponent set his hand at Dar es Salaam this 28th day of October, 2000.

SIGNED AND DELIVERED by the said
NTUMIGWA MOSSES MWAMPOONDELE
who is known to me personally
in my presence at Dar es Salaam
this 28th day of October, 2000.

Before me:

Commission for Oaths